

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
6 Septemba 2008**

**Waliohudhuria**

Aseli Wilison  
Bashiri Rashidi  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Husein Hamza Hamisi  
Hussein Idda Mkopi  
Juma Ali Salehe Jongo  
Mohamedi Saidi  
Mussa Alex  
Paulo Atibu Hatibu  
Pendo January  
Ramadhani Rajabu Nyengo  
Shamte J Kigoma  
Sosthenes C Amlima

**Ofisi**

Kazi ya kupaka rangi ya jina la UWABA nje ya ofisi imeshakamilika wiki tatu iliyopita. Benchi zimetengenezwa kwa ajili ya ofisi – gharama ilikuwa Tsh 50,000.

**Wamba Memorial Fund – Mradi wa Usalama Barabarani**

Wiki mbili iliyopita tulipiga video ya usalama wa baisikeli, na Amar alitumia video kamera yake. Ameshaondoka nchi na atatutumia kwa kupitia intaneti.

Kwa sababu ya kazi kubwa kutayarisha kwa ajili ya msafara wa baisikeli tulikubali kuendelea na mradi wa Wamba baada ya msafara kumaliza.

**Kibwana**

Juma alimpa Kibwana Tsh 35,000 kutengeneza baisikeli ya mlemavu wake. Kibwana alioa na Juma alihudhuria harusi.

**Kongamano**

Wiki ijayo tulikuwa na mkutano maalum kuhusu kongamano la kila mwezi. Elaine aliwasiliana na Diwani Lupilya kuomba ushauri wake na alisema atatupigia simu baadaye. Pia tumeomba ushauri wa Mbunge Azzan Zungu kwenye barua moja pamoja na maombi awe mgeni rasmi kwenye msafara.

**Rais**

Juma alipeleka barua kwa ofisi ya Rais Kikwete.

## **Umoja wa Ulaya**

Elaine aliwasiliana na wabunge wa bunge ya Ulaya kufuatalia kwa nini hatujapata jibu la barua letu kutoka ofisi ya umoja wa Ulaya hapa Tanzania. Mfanyakazi wa mbunge mmoja alifuatalia na aliweza kupata jibu kutoka ofisi ya umoja wa Ulaya Tanzania, ambayo alitutumia sisi. Elaine ataiprint na ataleta kwenye mkutano wa wiki ijayo.

Pendekezo moja ni kwamba UWABA tuhakikishe tupo kwenye orodha ya washika dau Wizara ya Miundombinu. Tulikubali kwamba tutajaribu tena kuwasiliana na Wizara hata baada ya jinsi mbaya walitutupia nje ya ofisi mara ya mwisho tulijaribu kutana na idara ya usalama barabarani ya Wizara.

## **Msafara wa Baiskeli**

Amar alifuatilia udhamini kutoka Vodacom lakini walisema kawaida wangenda kudhamini lakini wameshamaliza badjeti ya mwaka huu ya udhamini wa aina hii.

Mpaka sasa tumewasiliana na Ubalozzi wa Ireland, Ubalozzi wa Uholonzi, CRDB, NMB, Bakhresa, Ultimate Security na kampuni ya guta, na Juma alitembelea ofisi hizi tena kufuatalia. Elaine atafuatalia kwa simu wiki hii.

Elaine aliandika barua kuomba Mbunge Azzan Zungu awe mgeni rasmi yetu.

## **Mkutano wa gTKP kuhusu utawala wa usafiri, Cameroon**

Elaine alitumia maombi ya nafasi ya watu watatu kuhudhuria mkutano huu Cameroon – Mejah, Sosthenes na Filbert. gTKP walimchagua Mejah an wameshatayarisha usafiri wake. Elaine na Mejah wataandaa mada wiki hii na watapitia na wanachama wengine wiki ijayo.

## **Traffic Police**

Elaine aliandika barua kwa traffic police kuomba taarifa kuhusu operation kukamata magari yanayopaki kwenye service roads na kupendekeza watangeze kwenye vyombo vya habari. Sosthenes alifanya marekebisho na Juma na Paulo ataipeleka wiki hii.

## **Daraja la Kigamboni**

Elaine aliandika barua kwa NSSF kuomba taarifa kuhusu vipi tunaweza kutoa mapendekezo kuhusu daraja la Kigamboni, ambalo NSSF wanatoa fedha. Sosthenes alifanya marekebisho na Juma na Paulo ataipeleka wiki hii.

## **Mambo ya hela**

Elaine na Juma walichukua Tsh 120,000 kutoka benki. Tsh 50,000 ilitumikwa kwa benchi, Tsh 35,000 kwa Kibwana, Tsh 10,000 kwa chakula na soda za wageni wiki jana, Tsh 750 kwa bahasha, Tsh 500 kwa fagio kusafisha ofisi na Tsh 200 kwa upepo wa baisikeli ya Juma. Tulikata Tsh 20,000 ya posho ya Juma ya mwezi wa Septemba. Juma sasa anabaki na Tsh 41,700 ya hela ya UWABA.

**Mambo mengine**

Tuliongea kwamba ni vizuri kugawana zaidi kazi kati ya wanachama. Paulo na Edgar walijitolea kusaidia Juma katika kazi kusambaza na fuatalia barua. Elaine alisema atatafuta nafasi kufundisha kompyuta kwa wanachama ili waweze kuchapa barua.